

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Anuani ya Simu: "TAMISEMI"

Simu Na: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420

Nukushi: (026) 2322116, 2322146
2321013

Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa,
Jengo la Mkapa,
2 Barabara ya hospitali,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

TANGAZO LA KUITWA KAZINI

OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inapenda kuwataarifu waombaji kazi wa nafasi mbalimbali za kada za Afya walioomba kazi kuanzia tarehe **10/05/2018** hadi tarehe **25/05/2018** kuwa mchakato wa kuwapangia vituo vya kazi umekamilika.

Waombaji wote wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

- i) Waombaji wote wanatakiwa kuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Aidha waombaji watakaoshindwa kuripoti kwenye vituo vya kazi ndani ya siku kumi na nne (14) nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine haraka iwezekanavyo.
- ii) Waombaji wote wanatakiwa kuwasilisha vyeti halisi (**Originals Certificates**) vya kidato cha nne, sita, chuo, NACTE na vyeti halisi vya usajili wa mabaraza ya kitaalamu kwa ajili ya kuhakikiwa na mwajiri kabla ya kupewa barua ya ajira.
- iii) Waombaji waliopata nafasi za ajira wanajulishwa kuwa hakutakuwa na nafasi ya kubadilisha vituo vya kazi walivyopangiwa. Watakaoshindwa kuripoti katika muda uliopangwa, nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine wa kada husika.

Waombaji wote ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili, watambue kuwa hawakupata nafasi hivyo wasisite kuomba kwa mara nyingine nafasi za kazi zitakapotangazwa.

Waajiri wote mnaelekezwa kuwapokea, kuhakiki vyeti na kuwafanyia mafunzo elekezi (Induction Course) kabla ya kuwapangia vituo vya kazi.

Orodha ya majina ya waliopangiwa vituo vya kazi inapatikana kupitia tovuti ya OR-TAMISEMI www.tamisemi.go.tz.

Limetolewa na:-



Mathew Kwembe

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini
OR - TAMISEMI**

09/07/2018